# ACHIEVERS FOCUS EXAMINATION SERIES

WEGO PUBLISHERS
The achievers focus

## DARASA LA 7 – 2021
## KISWAHILI

005

**Muda: Saa 1 Dakika 40**

**Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne. Chagua jibu lifaalo zaidi kati ya yale uliyopewa.**

Ni habari __1__ kwamba matumizi ya mtandao __2__ kuongezeka nchini. __3__ zinaonyesha kufikia sasa, wakenya zaidi ya milioni kumi __4__ mtandao. __5__ kuwa wakenya zaidi ya ishirini elfu hutumia mtandao kwa siku. Idadi hiyo __6__ kuongezeka maradufu na kwa kasi __7__ kukamilishwa kwa mradi wa kuliunganisha taifa kwa kebo ya chini ya maji. Mtandao huinua __8__ vya maendeleo kupitia elimu, afya, biashara na kilimo ambacho ni __9__ wa taifa __10__ .

1. A. Jema B. Mbaya C. Njema D. Zuri
2. A. Inaendelea B. Zinaendelea C. Zitaendelea D. Yanaendelea
3. A. Idadi B. Takwimu C. Maarifa D. Nambari
4. A. Inatumia B. Wanatumia C. Wanatumiwa D. Tunatumiwa
5. A. Inakadiriwa B. Wanafikiria C. Tunakadiria D. Wanawazia
6. A. Inatakia B. Zinatarajiwa C. Inaruhusiwa D. Inatarajiwa
7. A. Kabla ya B. Baada ya C. Pindi D. Baadaye
8. A. Kiwango B. Shughuli C. Viwango D. Vikundi
9. A. Maarufu B. Uti wa mgongo C. Muhimu D. Msaada
10. A. Yetu B. Zetu C. Kwetu D. Letu

Mwenyezi Mungu alifanya kazi yake ya uumbji sawasawa. Alimpa binadamu __11__ ya kuwa mtunzaji wa viumbe wengine. Binadamu amegeuka __12__ kwa kutumia mazingira yake__13__. __14__ katika miji na vijiji huwa na takataka ambazo __15__ kote.

11. A. Dhima B. Lengo C. Jukumu D. Wajibu
12. A. Razini B. Timamu C. Hodari D. Hayawani
13. A. Visivyo B. Vilivyo C. Vyema D. Ipasavyo.
14. A. Yamkini B. Pengine C. Yakini D. Kumbe
15. A. Imesambaa B. Zimezambaa C. Zimejumuika D. Zimevunjika

**Kutoka swali la 16 – 30, chagua jibu sahihi.**

16. Ni sentensi ipi iliyo katika hali tegemezi?
    A. Wao hutuzwa kila baada ya kushinda
    B. Angesoma kwa bidii angefaulu
    C. Aliondoka kuelekea mjini
    D. Ukimwona mwalimu msalimie

17. Eleza matumizi ya ki katika sentesi ifuatayo.
    Kitoto kimeanguka kikicheza
    A. Ngeli B. Wakati C. Udogo D. Tendo kuendelea

18. Ukikosea mwezako bila kukusudia utamwambia
    A. Samahani B. Simile C. Pole D. Sitarudia

19. Tumia kiashiria radidi cha karibu
    Jina hilo ni la kibogoyo
    A. Huyu huyu B. Yuyu huyu C. Kiki hiki D. Yuyo huyo

20. Chagua sentensi iliyo katika muda mfupi uliopita.
    A. Alienda nyumbani
    B. Ameenda nyumbani
    C. Atakula hadi ashibe
    D. Anacheza na watoto

21. Andika wingi wa
    Seremala huyu wangu ana kufuli
    A. Seremala hawa wetu wana makufuli
    B. Maseremala hawa wangu wana makufuli
    C. Maseremala hawa wetu wana makufuli
    D. Seremala hawa wetu wana vifuli

22. Mvua, sukari, maziwa, asali ni mfano wa nomino
    A. Makundi B. Fungamano C. Jumla D. Dhahania

23. Tumia kiunganishi kifaacho kujazia pengo.
    Mwanafunzi hataingia darasani----idhini ya mwalimu
    A. Ghairi ya B. Bali C. Mathalani D. Japo

**24.** Salamu zipi zilizoambatanishwa vyema?
A. Alamsiki – majaliwa
B. Lala unono – jaala
C. Shikamoo – nawe pia
D. Usiku mwaka – wa mafanikio

**25.** Utamwitaje kaka wa mke wako?
A. Wifi B. Mkoi C. Mpwa D. Mwamu

**26.** Neno 'karai' liko katika ngeli gani?
A. I-ZI B. LI-YA
C. U-ZI D. I-I

**27.** Neno jingine lenye maana sawa na utepetevu ni
A. Uzembe B. Upotovu
C. Ulaghai D. Uhodari

**28.** Ipi ni sahihi kisarufi na kimantiki?
A. Shambani kule pana mimea mingi
B. Shuleni humu mna wanafunzi wengi
C. Duka pale pana bidhaa
D. Tutaenda shule kesho

**29.** Kamilisha methali: adui aangukapo
A. Mmalize B. Mpige
C. Mnyanyaze D. Mnyanyue

**30.** Tambua vazi linalovaliwa na wanaume
A. Kanchiri B. Shimizi
C. Bombo D. Blauzi

**Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali 31-40.**

Ipo siku nitakufa, na mauti kunifika,
Nitafikwa na maafa, roho yangu kutoweka,
Pindi nitakapokufa, kule kwangu mtafika,
Kifo change nikawaza, ni mauti si kulala

Marafiki watafika, ushuhuda kuutoa,
Sifa zangu tasikika, twamjua hana doa,
Hakika hawatataka, siri zangu kuzitoa,
Kifo changu nakiwaza, ni mauti si kulala.

Maadui wana lao, mazishini watafika,
Kulitupa jicho lao, kama kweli nimekonda,
Watasifu mungu wao, sala zao kukumbuka,
Kifo changu nakiwaza, ni mauti si kulala.

Majirani watasifu, nilivyokuwa mpole,
Watautaja wasifu, kunisemea kongole,
Watamtakia mfu, pumziko la milele,
Kifo changu nakiwaza, ni mauti si kulala.

Na sanda watanivika, kwenye kiza kuniweka,
Jeneza watalizika, na kaburi kufunika,
Mifupa nitageuka, jina kusahaulika,
Kifo changu nakiwaza, ni mauti si kulala.

**31.** Shairi hili ni la aina gani?
A. Tathlitha
B. Tarbia
C. Tathnia
D. Tasdisa

**32.** Shairi hili lina mishororo mingapi
A. Ishirini
B. Arubaini
C. Mine
D. Mitano

**33.** Ni msamiati upi tofauti?
A. Deuli
B. Jeneza
C. Sanda
D. Insafu

**34.** Je, taja mloto wa ubeti wanne.
A. Majirani watasifu, nilivyokuwa mpole
B. Pindi nitakapokufa, kule kwangu mtafika
C. Watamtakia mfu, pumziko la milele
D. Watautaja wasifu, kunisemea kongole

**35.** Marafiki na maadui wanatofautiana vipi kulingana nashauri hili
A. Shabaha zao tofauti
B. Jinsi wanavyozigana
C. Macho yao tofauti
D. Kutokuwa na siri

**36.** Je, kitabu cha mashairi huitwaje?
A.Kishairi B. Diwani
C. Shayara D. Ramani

**37.** Na sanda watanivika kwenye kiza kuniweka. Kiza hapa chamaanisha nini?
A. Kaburi B. Usiku C.Kifo .D. Sanda

**38.** Ni nini husomwa wakati wa mazishi kulingana na shairi hili?
A. Vitambulisho
B. Historia ya mfu
C. Watu wa familia
D. Wasifu wa mwendazake

**39.** Kwa nini mwandishi anawaza kifo chake? Kwa sababu.
A. Majirani watalia
B. Kifo hakina marejeo
C. Kwa sababu ya maadui
D. Siri hazitajulikana

**40.** Kipokeo cha ubeti wa kwanza ni kipi?
A. Ipo siku nitakufa, na mauti kunifika
B. Kifo changu nikiwaza, ni mauti si kulala
C. Pindi nitakapokufe, kule kwangu mtafika
D. Nitafikwa na maafa,roho yangu kutoweka

**Soma taarifa hii kisha ujibu maswali 41-50.**

Aisha na Anita walikuwa mji wa Raha tele. Walijuta walivyodanganywa kuja hapa. Maisha yalikuwa yamewaendea segemnege. Aisha alikuwa sasa ameshakasirika kuliko Anita. Alimsikitikia sana mwenzake.

Ukiwa ulianza kumvaa Anita. Alionekana kama ua zuri lililosongwa na miiba jangwani, Aisha aliyainamisha macho yake kwa masikitiko lakini hasa akiepuka kulitazama lile chozi lililomtoka Anita na kuanza kumtiririka shavuni. Mwenyewe alikumbuka taswira ya baba yake; lakini pichani tu. Picha aliyoibeba kumkumbusha tu kuwa hata yeye alitoka katika jamaa fulani. Jamaa ambayo isingeweza kumsitiri na mapigo ya malimwengu ya walimwengu ulimwenguni.

Sijui ni kwa nini baba hakunilipia karo nikasoma. Nilifuzu vizuri nikapokea mwaliko wa kujiunga na shule ya upili Songambele. Eti kumwelimisha msichana ni kazi bure, angeolewa aende zake kumfaa mume na wakwe zake. Hivyo basi akaamua kuizamisha rasilimali yake katika ulevi. Kweli cha mlevi huliwa na mgema na cha baba hakikuliwa tu bali kiligugunwa hata mifupa isibaki chochote. Aligeuka kuwa mtumwa aliyeitwa akaitika na huko ndiko alikoishia

Cha kuvunda hakina ubani. Baba aliipiga dunia teke baada ya kubugia mtindi wenyewe mchanganyiko wa kemikali ya kuhifadhi wafu makafani..." sasa machozi yalimbubujika tu laiti ningalisoma! Eti badala ya masomo nichumbiwe, niingie unyagoni nikeketwe nifunzwe kunga za unyumba kisha niozwe. Nitolewe mahari ya kuwafaidi baba na aila zangu japo mazumbukuku. Aisha, maini yananikatika niwaonapo wanawake maarufu waliomudu kusoma wakajipangia mikakati ya kujiendeleza na kuyaboresha maisha yao, jamaa na jamii kwa jumla. Wanawake maarufu katika rubaa za kimataifa. Namuenzi marehemu profesa Wangare Maathai na wengine. Ni kweli uongo wa wanaume, umewaua wasichana na kuwazika na ndoto zao

Hakika uwaonapo wanaume, huwezi kujua ni msururu wa makaburi mangapi ya ndoto za wasichana yanawafuata nyuma yao. Suala nyeti ni matatizo yaletwayo na udhalimu huu yatamalizika lini?

**41.** Tunaweza kusema Aisha na Anita ni :
A. Rafiki wa toka nitoke
B. Marafiki wa kufa kuzikana
C. Ndugu wa tumbo moja
D. Adui wakubwa

**42.** Anita:
A. Alikuwa mfano wa ua zuri jangwani
B. Alitoka katika jamaa ya walala heri
C. Alitoka katika jamaa ya mzazi pweke
D. Alitoka katika jamaa ya uchochole

**43.** 'Kumuelimisha msichana ni kazi bure' je maneno haya ni sawa kulingana na ufahamu uliosoma
A. Sawa kabisa
B. La hasha
C. Labda
D. Sijui

**44.** Methali 'cha mlevi huliwa na mgema'. inadhihirika katika:
A. Babaye Anita kuajiriwa kuhifadhi maiti
B. Anita kuolewa na kuwafaa wakwe zake
C. Baba kuzamisha rasilimali yake kwa kupiga mtindi
D. Babake Anita kufariki

**45.** Kulingana na taarifa ni ipi isiyokuwa dhuluma dhidi ya mabanati?
A. Kuchumbiwa, kukeketwa na kuingizwa unyagoni
B. Kufundishwa kunga za unyumba na kuozwa.
C. Kulipiwa mahari ya kuwafaidi baba na kaka
D. Kushinikizwa kwenda shuleni ili kuifaidi jamii.

**46.** Mwandishi anamaanisha nini anaposema <u>kiligugunwa hata mifupa isibaki?</u>
A. Kukimu jamii yake vyovyote vile
B. Kuishiwa kwa baba Anita na kubaki hohehahe
C. Kuwafaa mume na wake zake
D. Kufuzu vizuri kwa Anita shuleni

**47.** Kwa mujibu wa taarifa, Bi, Wangari Maathai:
A. Ni mmojawapo wa wanawake wasiotajika
B. Ni mmojawapo wa walionyimwa haki zao
C. Ni mmoja wa marafiki wa Anita
D. Ni mmoja wapo wa walioboresha maisha ya jamii

**48.** Anita anamwambia Aisha "maini yananikatika" kwa sababu:
A. Alikuwa amewezwa na uongo wa wanaume
B. Alikuwa na uwezo wa kuifaa jamii Zaidi
C. Alikuwa amenyimwa mahari ya kumfaa baba
D. Alikuwa akiwalilia ngoa wanawake waliofaulu

**49.** Kulingana na taarifa, Anita alisoma hadi kiwango kipi?
A. Kidato cha pili
B. Kidato cha nne
C. Darasa la nane
D. Chuo kikuu

**50.** Methali inayoafiki taarifa hii ni:
A. Aisifuye mvua imemnyea
B. Mwenye nguvu mpishe
C. Mwerevu hajinyoi
D. Kinolewacho hupata